SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.21 NO. 1 2022
DOI: 10.51984/JOHS.V21I1.1483

مجلة جامعة سبها للعلوم الإنسانية
Sebha University Journal of Human Sciences

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs

# Taswira Ya Mapenzi Katika Nyimbo Za Watanzania

Mohamed Musbah Ali Mohamed

African Languages, Faculty of Arts, Sebha University, Libya

**Keywords:**
Taswira
Nyimbo
Matumizi
Takriri
Mapenzi.

**A B S T R A C T**

Makala hii inabainisha taswira ya mapenzi kama inavyojitokeza katika nyimbo teule za Mzee Yusuf Mzee. Katika kufanikisha lengo hili, taswira ya mwanamke iliyobainishwa ni pamoja na mapenzi ni upendo, mapenzi na fitina, mapenzi ni kujiamini, mapenzi na dua, mapenzi ni kutendeana wema na mapenzi na tabia nzuri. Pia makala hii hubainisha uhalisia wa taswira ya mwanamke inayojitokeza katika nyimbo teule za Mzee Yusuf Mzee kwa jamii ya leo.

# صورة عاشق في الأغاني التنزانية.

محمد مصباح على محمد

قسم اللغات والدراسات الإفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
تشبيه
أغانى
إستخدامات
تكرار
الحب

**الملخص**

يستكشف هذا المقال صورة الحب كما تظهر في الأغاني المختارة لمزي يوسف مزي. ولتحقيق هذا الهدف فإن صورة المرأة التي تم تحديدها تشمل الحب هو الحب و حب ومكائد ، والحب ثقة بالنفس وحب ودعاء، الحب هو معاملة بعضنا بعضاً باللطف والحب والسلوك الحسن. يسلط هذا المقال الضوء أيضًا على حقيقة صورة المرأة الناشئة في الأغاني المختارة لمزي يوسف مزي في المجتمع اليوم.

## 1.1 Matumizi ya Misemo

Misemo ni moja kati vipengele vya matumizi ya lugha kinachopatikana katika utanzu wa semi ambacho hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi kuwasilisha maudhui kwa hadhira iliyokusudiwa. Misemo hurejelea kauli fupi fupi zenye kuakisi jambo kama lilivyo au linavyotakiwa kuwa kulingana na muktadha maalumu (Mlacha, 1996). Tunasema muktadha maalumu kwa sababu ipo misemo ya kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni, kijamii, kimapenzi na kitaaluma pia. Taarab ya mipasho, kama ilivyo ile ya Mzee Yusuf Mzee, imesheheni matumizi makubwa ya misemo ambayo mara nyingi inatumika katika kuwapasha watu wanaochukia kuona wawili wanaopendana wanadumu katika mapenzi yao kuwa hawawezi kuwatenganisha. Mfano mzuri wa matumizi ya misemo unajitokeza katika wimbo wa *Kipendacho Roho hula nyama Mbichi*. Mtunzi anasema:

Mkisema ni mbaya, kwangu mimi ni king'asti
Kwa anayoniridhia, kumuacha si rahisi
Maradhi nikiugua, yeye ndiye wangu nesi
Dozi ananipatia, kwa huduma ni mwepesi
Kila nikihitajia, sitamki anahisi
Huba zake maridhawa, kuzikosa sidiriki

Twaitana kiungwana, sio we baba fulani
Yeye bibi mimi bwana, au sweet or honey
Ni mwiko kurushiana, maneno kihunihuni
Maraha tunapeana, nyama za ndimi laini
Ndo haya mkiyaona, mnakatika maini

*Corresponding author:
E-mail addresses: moh.mohamed1@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 24 September 2021 - Received in revised form 29 March 2022 - Accepted 03 April 2022*

Basi mtaumwa sana, la kwetu hamlipati
Kiitikio
Kipendacho roho, hula nyama mbichi
Mtaanzisha mbio, huyu simuachi
Ni langu chaguo, ameshanitachi

Katika dondoo hili mtunzi ameanza kwa kueleza namna yeye na mpenzi wake wanavyopendana na kwamba kila kitu anachotaka anakipata kutoka kwa mpenzi wake. Katika kuthibitisha hilo, anasema, "dozi ananipatia, kumuacha si rahisi na maradhi nikiugua yeye ndiye wangu nesi." Kauli hii inaonesha kuwa kisaikolojia tayari Mzee Yusuf Mzee amesharidhika na mapenzi yote anayopewa na mkewe na kwamba hata wafitini wafanye nini hawawezi kuwatenganisha kamwe. Katika hali ya kawaida, saikolojia ya mwanadamu inapokubaliana na jambo fulani ni vigumu sana kurudi nyuma ndio maana mtunzi anatumia msemo kuwa, "kipendacho roho, hula nyama mbichi." Msemo huu una maana kubwa sana katika ulimwengu wa mapenzi ambapo kama watu wawili wamependana, hakuna mtu mwenye uwezo wa kuwatenganisha kwa sababu kile kilichowafanya wapendane ni wao wenyewe tu ndio wanaokifahamu (Ahearn, 2001). Katika hali ya kawaida, si rahisi kuona mtu anakula nyama mbichi kwani inaweza kumdhuru kiafya kwa sababu mfumo wa mmeng'enyo wa chakula wa binadamu haukubaliani na nyama mbichi kama ilivyo kwa baadhi ya wanyama kama simba, chui, fisi, mbwa mwitu, paka na wengineo.

Katika maisha halisia ya jamii, wapo baadhi ya watu ambao kazi yao kubwa ni kuhakikisha kuwa watu wengine, hasa wanaopendana, hawadumu katika mapenzi yao kwa muda mrefu. Hili ni tukio la kisaikolojia ambapo utaona baadhi ya watu hawajisikii vizuri kuona watu wanaopendana wanaishi kwa raha mustarehe na badala yake watafanya kila linalowezekana ili kuwatenganisha. Mtunzi anasema, "mkisema ni mbaya, kwangu mimi ni king'asti," kauli inayodhihirisha kuwa wapo watu ambao hawapendi kuwaona watu wanaopendana wakidumisha mapenzi yao. Jambo la msingi na muhimu ambalo wapendanao wanatakiwa kulifanya ni kutotoa nafasi kwa wafitini hao na badala yake wanatakiwa kuendeleza pendo lao kwa mahaba zaidi ili kuwakomesha (Khamis, 2004).

Mtunzi anaendelea kutumia misemo kuwasilisha dhamira juu ya namna penzi linavyotakiwa kulindwa na kuenziwa dhidi ya wafitini. Anatumia lugha ya kuwakatisha tamaa watu wote wasiolitakia mema penzi lao kwamba hata wafanye nini hawawezi kuwatenganisha. Haya yanapatiana katika wimbo wa *Tupendane* kama anavyosema:

Pendo tumelizingua, kwa Yasini tatu
Lisije kuhusudiwa, na macho ya watu
Yeye namuaminia, nami kumuacha sithubutu
Mbona mtaumwa sana, na vigumu kupona
Roho zitawasonona, sisi huku twawaona
Ni vigumu kuachana, ye tv mi antenna
Kama shubiri ni tamu, asali ina ladha gani
Huyu kanitia wazimu, vineno neno punguzeni
Kama mnaweza, pandeni juu mwende mkazibe
Mpande helkopta
Mpande ungo

Mtunzi anaonesha kuwa yeye na mpenzi wake wameshibana sana kiasi kwamba hakuna mtu wa kuweza kuwatenaganisha. Anasema, "ni vigumu kuachana, yeye tv mi antenna," akiwa na maana kuwa televisheni haiwezi kufanya kazi kama hakuna antenna. Hii ni sawa na kusema kuwa kwa vyovyote vile, hakuna anayeweza kuwatenganisha watu ambao wamependana kwa mapenzi ya dhati kabisa. Huu ni msemo wenye kuleta hisia na tafakuri katika saikolojia ya mtu yeyote ambaye kazi yake ni kufitinisha watu wanaopendana. Anaposikia msemo kama huu, hukosa nguvu ya kuendelea kufanya maovu na hila za kuwatenganisha watu wanaopendana. Katika ubeti unaofuata mtunzi anatoa msemo mwingine kuwa, "kama shubiri ni tamu, asali ina ladha gani," kwa lengo la kutoa msisitizo kuwa mapenzi yao ni ya dhati na hakuna mtu anayeweza kuyatenagisha. Mapenzi yao ni zaidi ya utamu wa asali na katika hali ya kawaida, asali ndicho kimiminika kilicho kitamu zaidi ukilinganisha na vingine. Msemo huu unayo nafasi kubwa ya kuingia katika saikolojia ya watu ambao ni wafitini na kuona kuwa harakati na mipango yote wanayoifanya kwa ajili ya kuwatenganisha wapendanao ni kazi bure na haiwezi kufanikiwa (Traore, 2004). Baada ya kulitambua hili, wataacha mara moja fitina na kulifanya penzi la wanaopendana liendelee kudumu na kunawiri.

**1.2 Matumizi ya Mbinu ya Takriri**

Takriri ni marudiorudio ya vipengele fulani katika kazi ya fasihi mara zaidi ya moja ukilinganisha na vipengele vingine katika kazi ya fasihi. Takriri huweza kujitokeza kama neno, sentensi au aya ambayo hurudiwa zaidi ya mara moja kwa lengo la kutoa msisitizo fulani juu ya jambo la msingi ambalo mtunzi analielezea (Yego, 2013). Wakati mwingine mtunzi wa kazi ya fasihi anaweza kurudia silabi fulani akiwa na lengo kutoa msisitizo au kutaka kitu fulani kifahamike na kionekane kwa haraka zaidi katika akili ya wasomaji. Hii ni sawa na kusema, upo uwezekano wa kupata takriri silabi katika kazi ya fasihi kama ilivyo katika nyimbo za taarab za Mzee Yusuf Mzee. Katika wimbo wake wa *Kipendacho Roho Hula Nyama Mbichi* kunajitokeza matumizi ya takriri kama ifuatavyo:

Imefika, imefika, imefika, saa na dakia zake
Imefika kuwaambia, wapambe sasa watoke
Huyu ni mpenzi wangu, hiki ni kichuna change
Huyu ni choisi yangu, huyu ni choisi yangu
Simuachi hata kwa ngumi, mapanga na majambia
Hamjui ananipa nini ee, hamjui ananitunza vipi

Hamjui ananipa nini, niacheni.

Takriri silabi "ngu" imejitokeza kwa kujirudia mara tatu katika ubeti uliopo hapo juu, ikiwa ni katika maneno mawili tofauti. Takriri hii imejitokeza katika maneno ya "wangu na yangu" ambapo neno "wangu" limejitokeza mara 2 na "yangu limejitokeza mara 1. Hii ni silabi ya kumilikisha ambayo inaonesha namna Mzee Yusuf Mzee alivyommiliki mpenzi wake kiasi kwamba hakuna mtu mwingine yeyote mwenye uwezo wa kuwatoa katika mapenzi yao. Waswahili wanao msemo wao usemao kuwa "mtu hujidai na chake," na hapa mtunzi anatuonesha namna anavyojidai na chake. Katika hali ya kawaida, kisaikolojia mtu huwa na amani ya nafsi katika mapenzi pale anapojiona kuwa yeye ni mmiliki wa mapenzi ya mwenzi wake na hakuna mtu mwingine ambaye anaweza kumwibia. Hali hii humfanya mtu kuwa na furaha muda wote na kuishi katika maisha ya amani na upendo. Lakini ile dhana ya kumiliki inapokosekana na mmoja kati ya wapenzi akadhani au akaona kabisa kuwa yeye si mmiliki wa mapenzi ya mwenzi wake, kuna mtu wa pembeni anayemwibia, maisha huwa machungu mithili ya shubiri. Hivi ndivyo namna saikolojia ya mwanadamu ilivyo, kamwe haikubali kuingiliwa katika masuala ya mapenzi na mtu mwingine wa nje.

Vile vile, katika dondoo lililopo hapo juu, kuna matumizi ya takriri neno ambapo neno "imefika," limerudia mara nne kutoa msisitizo kuwa sasa ule muda wa kumtambulisha mpenzi kwa watu umefika. Hii ina maana kuwa kuanzia kipindi hicho watu wote wanatakiwa kufahamu kuwa mpenzi wa Mzee Yusuf Mzee ndiye huyo anayetambulishwa na hakuna mwingine tena. Watu wote wenye nia mbaya na wanaodhani kuwa wanaweza kumyumbisha kimapenzi, hapo tena ndo wafahamu kuwa yeye tayari amempata mwandani wake. Wanawake wote ambao walikuwa wanammezea mate Mzee Yusuf Mzee wanatakiwa kutambua kuwa mwisho wao umefika na yeye sasa anaye mpenzi wake na hataki tena kusumbuliwa na kufuatiliwafuatiliwa na wanawake wengine.

Katika mistari miwili ya mwisho katika ubeti uliopo hapo juu, mtunzi ametumia takriri sentensi, "hamjui ananipa nini," kwa kuirudia sentensi hii mara mbili. Takriri hii imetumika katika kutoa msisitizo wa kwamba, mapenzi ni kuridhiana na kuridhika na kile ambacho wapenzi wanapeana. Ikiwa wapenzi wataridhika na mapenzi yao ni wazi kuwa wataifanya ndoa yao iweze kudumu na hakuna mtu ambaye ataweza kuwavurugia mapenzi yao. Nadharia ya Saikolojia Changanuzi inatufahamisha kuwa hakuna kitu kilicho bora kama kuridhika na jambo kwani huifanya nafsi kutulia na kutoyumbishwa na mambo mengine yenye nia ya kuharibu (Sternberg, 1986).

Matumizi mengine ya takriri yanajitokeza katika wimbo wa *Linawachoma* mwishoni mwa kiitikio cha wimbo huu. Mtunzi anasema:

Donge hilo donge, donge hilo wanaona donge
Waona donge la nini, sisi tumeshashibana
Hata mkifanya nini, ni muhali kuachana
Sisi tumeshaamua, hatuataachana katu
Tena tumelizingua, pendo kwa Yasini tatu

Neno "donge" limerudiwa mara tano katika dondoo lililopo hapo juu huku mara nne ikiwa ni katika msitari mmoja na mara moja katika msitari wa pili. Neno hili maana yake ya msingi ni wivu au husuda ambapo mtu mmoja au kikundi kinaweza kumfanyia mtu mwingine au kikundi. Kutumiwa hapa neno hilo kunaashiria kuwa katika jamii wapo watu ambao huwaonea wivu watu wanaopendana na kufanya kila wanaloweza ili kuwatenganisha. Hata hivyo, katika dondoo hili kunabainishwa kuwa wenye donge tayari wameshafahamika na kwamba hata wafanye nini donge walilonalo haliwezi kusababisha watu wanaopendana kutengana. Ni jambo la kawaida katika jamii kuona baadhi ya watu wakiwa na husuda na wivu kwa watu wanaopendana. Nadharia ya Saikolojia Changanuzi inatufahamisha kuwa kwa asili binadamu ni kiumbe mbinafsi na hivyo hapendi kuona watu wengine wanaishi kwa amani bali yeye tu ndiye anayestahili kuishi maisha mazuri yaliyojaa mapenzi. Hata hivyo, njia pekee itakayowafanya wale wanaopendana kuendelea kuishi maisha yenye upendo na mapenzi ni kutosikiliza maneno ya watu na waendelee kusonga mbele katika mapenzi yao.

**1.3 Matumizi ya Lugha ya Mafumbo**

Matumizi ya lugha ya mafumbo ni sifa muhimu inayopamba na kujitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za taarab, hususani taarab asilia na taarab ya mipasho pia (Mgana, 1991). Lugha ya mafumbo ni ile ambayo hutumika kuelezea mambo kwa kufichaficha bila ya kusema kwa uwazi. Sababu za kutumia lugha ya mafumbo ni nyingi, lakini kubwa zaidi ni kumfanya msomaji au msikilizaji wa kazi ya fasihi kutafakari kidogo kile anachokisikia au kukiona ndipo ayapate maudhui yaliyokusudiwa (Mwamzandi, 2001). Na ndipo sasa kila hadhira ya kazi ya fasihi inaweza kupata maudhui ambayo ni tofauti na mwenzake kwa sababu kila mmoja anaweza kufumbua fumbo lililowasilishwa mbele yake kwa namna tofauti na mwingine. Sababu nyingine ya kutumia lugha ya mafumbo katika kazi za fasihi ni kuficha ukali wa maneno ambayo kiutamaduni hayafai kusemwa waziwazi mbele za watu. Mathalani, masuala yanayohusiana na mapenzi hayapendezi kusemwa waziwazi mbele za watu kwa sababu ni masuala ya ndani yanayopendeza kusemwa na watu wawili wawapo katika faragha.

Mzee Yusuf Mzee ametumia matumizi ya lugha ya mafumbo kwa kiasi kikubwa sana katika nyimbo zake kwa lengo lile lile la kumfanya msomaji afikiri kidogo kabla ya kupata maana na pia kuficha ukali wa mambo ambayo hayapendezi kusemwa mbele za

watu waziwazi. Katika wimbo wa *Tupendane* anasema:

Ooo habibit wangu, usipunguze dozi mi bado sijapoa
Ooo daktari wangu, dawa zako wewe ndo zitonisaidia
Sweet asubuhi nikiwa hoi, kwa ya jana makamuzi
Honey basi nipikie chai, yenye nyingi tangawizi
Tutoke tukatanuwee, popote katika nchi
Popote wee nambie, White Sandy, Koko beach
Kisha nitayarishie, juice ya parachichi
Wazushi tuwaringie, timu yetu kali kwa mechi.

Katika dondoo hili mtunzi ametumia lugha ya mafumbo pale aliposema, "ooo daktari wangu, dawa zako wewe ndo zitonisaidia, sweet asubuhi nikiwa hoi, kwa ya jana makamuzi, honey basi nipikie chai, yenye nyingi tangawizi." Hapa ametumia lugha ya mafumbo kurejele tendo la ndoa baina ya mtu na mpenzi wake. Maneno yaliyotumika katika dondoo hili yanaweza kufahamika maana yake kwa watu wazima peke yao huku watoto wakiambulia patupu pale wasikiapo maneno haya. Kwa kiasi fulani, taarab ya Mzee Yusuf inajitahidi kutumia lugha ya mafumbo licha ya kuwa moja kati ya sifa ya nyimbo za taarab ni kutumia lugha isiyokuwa ya kificho (Khamis, 2007).

**1.4 Matumizi ya Balagha**

Balagha ni mbinu ya matumizi ya lugha ambapo mtunzi wa kazi ya fasihi huitumia katika kueleza mambo kwa kuyakuza zaidi kuliko uhalisia wake ulivyo (Yego, 2013). Kwa maneno mengine, matumizi ya lugha ya balagha hufahamika kama chuku, yaani kukoleza chumvi katika kueelezea jambo. Matumizi ya mbinu hii ya kisanaa hutumiwa na watunzi wa kazi za fasihi katika kuonyesha msisitizo wa jambo ulivyo. Mzee Yusuf Mzee ametumia mbinu hii katika kuwasilisha dhamira ya mapenzi katika nyimbo nyingi, lakini ile ya *VIP Soda ya Kopo* ni mfano mzuri. Katika ubeti wa tatu anasema:

Jamani nahudumiwa, raha hadi utosini
Nnachotaka napewa, niseme nataka nini
Raha singoji kupewa, najipa mwenyewe jamani
Naona ntachelewa, kidume kula maini
Chakula nnapikiwa, nnawekewa mezani
Nikila nnapewa, kishuke vyema tumboni
Sigombwi mimi nadekezwaa
Kufanya utundu, nakatazwaa
Siwahi kusema, naulizwaa.

Katika msitari wa kwanza wa ubeti huu, mtunzi anatumia mbinu ya balagha kuonyesha namna anavyoridhishwa na mpenzi wake. Anaeleza kuwa, "jamani nahudumiwa, raha hadi utosini," akimaanisha kuwa mapenzi anayopatiwa na mapenzi wake ni ya kiwango cha hali ya juu kabisa. Si jambo la kawaida kwa mtu kusikia raha hadi utosini bali katika ulimwengu wa balagha hilo linawezekana (Khatib, 1992). Kwa mujibu wa nadharia ya Saikolojia, inaelezwa kuwa, mwanadamu anapokuwa katika hali ya kuridhika katika mapenzi humfanya kujiamini na kumpenda zaidi mpenzi wake na hatimaye kudumisha mapenzi yao (Rahim, 2002). Hapa, wapendanao wanafahamishwa kuwa ni vema wakayaendeleza mapenzi yao kwa kuhakikisha kuwa wanaridhishana kimapenzi na hata kwa mahitaji mengine pia. Ikiwa mmoja kati ya wapenzi hawezi kumridhisha mwenzake, ni wajibu wao kuwa na ubunifu ambao utawezesha kuridhishana.

Matumizi ya mbinu ya balagha yanajitokeza pia katika wimbo wa *Nakula kwa Nakshi Nakshi* kupitia katika kiitikio cha wimbo. Mtunzi anasema:

Jamani kupendana raha, walimwengu msisikie
Najidai hadi raha, mradi msinisogelee
Kwenye raha tunaishi, kama hatuko duniani
Nakula kwa nakshi nakshi, naogelea pendo.

Msitari wa tatu katika kifungu hapo juu, ndio ulitumia mbinu ya balagha katika kuelezea namna mapenzi baina ya mtunzi na mpenzi wake yalivyo matamu. Maneno kuwa, "kwenye raha tunaishi, kama hatuko duniani," ni maneno yaliyojaa lugha ya kibalagha. Maana ya balagha hii ni kuwa mapenzi na starehe wanazozipata wawili hao wanaopendana, ni sawa na zile ambazo zinapatikana Peponi. Katika mafundisho ya dini, hususani dini ya Kiislamu, kunaelezwa kuwa watu watakaoishi maisha ya dunia kwa kufanya ibada na kuwa watu wema watakwenda kuishi maisha ya starehe zaidi huko peponi. Inaelezwa kuwa huko Peponi kuna wanawake wazuri wasio na mfano wakiitwa Mahurilain na pia wanaume watapewa nguvu ambazo zitawawezesha kutochoka wakati wakiwa katika tendo la ndoa. Kwa mujibu wa nadharia ya Saikolojia Changanuzi, inaelezwa kuwa mtu anapokuwa na uhakika kuwa mapenzi anayopata hapa duniani yanafanana na yale ya peponi, anajijengea hali ya kudumu katika mapenzi na mpenzi wake aliyenaye kwa sasa. Wanajamii wanashauriwa kuamini kuwa mpenzi aliyenaye anaweza kumpatia mapenzi mujarabu na kupata raha isiyo kifani katika maisha ya duniani.

**1.5 Matumizi ya Sitiari**

Sitiari ni moja kati ya mbinu ya tamathali ya semi inayotumika katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira wa kazi za fasihi simulizi na andishi (Mlacha, 1996). Sitiari ni mbinu ya matumizi ya lugha ambayo hutumiwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa na tabia zinazotofautiana kana kwamba ni vitu vilivyosawasawa kabisa kwa kutumia viunganishi kama, "ni" katika sentensi, "Saidi ni nyoka." Hapa Saidi anafananishwa na nyoka kama ni vitu viwili vinavyofanana hali ya kuwa hivi ni vitu viwili tofauti kabisa. Hata hivyo, upo uwezekano wa sitiari kujengwa bila hata ya kutumia viunganishi vya aina yoyote ile bali maneno tu. Sitiari hutumiwa

katika kazi za fasihi kwa lengo la kutoa msisitizo juu ya dhamira ambayo fanani anataka hadhira yake iipate.

Msanii Mzee Yusuf ni bingwa wa kutumia sitiari tena zisizotumia viunganishi ambazo hasa ndizo zinazolandana na nyimbo za taarab ya Mipasho. Katika wimbo wa *Tupendane* ubeti wa pili kuna matumizi ya sitiari pale mtunzi anaposema:

Ooo mpenzi wangu, wabaya wetu macho watukodolea
Oooh tuzidi kuomba Mungu, penzi letu lizidi kumea
Honey nataka unibebe, unipeleke kuoga
Sweet nilishe nishibe, hata mlo uso mboga
Kisha nikupe kila kitu, ulichohalalishiwa
Nami nikupe mavitu, mwenyewe unanijua
Kisha tucheze sebene letu, mpaka jogoo anatuwa
Kwa kila mbaya wetu, kituona atazimia.

Kifungu cha ubeti hapo juu kina matumizi ya sitiari katika msitari wa tatu na wa nne ambapo maneno kama vile “Honey” na “Sweet” ndiyo yaliyotumika kisitiari. “Honey,” ni neno la Kiingereza linalojulikana kama asali kwa lugha ya Kiswahili. Hapa mwanamke anafananishwa na asali ikiwa na maana kuwa asali ni tamu na kwamba mapenzi anayopatiwa na mpenzi wake ni matamu kama vile ulivyo utamu wa asali. Neno “sweet,” ni la Kiingereza linalojulikana kama “peremende,” kwa lugha ya Kiswahili. Peremende kwa kawaida ni kichangamsha mdomo ambacho kina sukari na hupendwa na watu wengi wakiwepo watoto. Katika dondoo hapo juu, peremende inafananishwa na mwanamke kana kwamba ni vitu viwili vilivyo sawa sawa kabisa (Yego, 2013).

Mawazo makuu ya nadharia ya Saikolojia yanathibitisha kuwa, pale wapenzi wanapoitana majina mazuri hata kwa kutumia jina la kitu kingine husaidia sana katika kujenga na kuishibisha Saikolojia. Majina kama “sweet” na “honey,” ni majina ya vitu vitamu; sasa ndo mwanamke amepewa majina haya na kwa hivyo yanamfanya mwanamke kuona kuwa yeye ni mtu wa thamani sana na anayo haki ya kujivunia uanawake wake (Boeree, 2006).

Matumizi ya sitiari tajwa hapo juu yanajitokeza katika beti za tatu na nne katika wimbo huo huo wa *Tupendane*. Hata hivyo, katika ubeti wa tatu kuna sitiari mpya inayojitokeza katika msitari wa kwa kwanza wa ubeti huo. Msitari huo ni ule usemao, “ooo ayuni wangu, raha ya mapenzi wazushi uwapuuze.” Neno “ayuni,” katika msitari huu lina maana ya ndege, lakini hapa si ndege bali ni mwanamke ndiye anayeitwa kwa jina hili. Ndege kuhusishwa na mapenzi si kitu kipya kwani ndege wengi kama tausi na njiwa wamekuwa wakitumiwa kisitiari hususani za mapenzi kwa muda mrefu katika kazi za fasihi. Katika ubeti wa nne msitari wa pili, anasema, “ooo daktari wangu, dawa zako wewe ndo zitonisaidia.” Hapa neno “daktari,” limetumika kisitiari ambapo mwanamke amefananishwa na tabibu anayetibu katika hospitali, zahanati au kituo cha afya. Kitendo cha mwanamke kuweza kumtimizia mumewe haja zake za kimapenzi zinafananishwa na ujuzi alionao daktari katika kutibu maradhi yanayowasumbua wagonjwa (Yego, 2013).

**2.1 Mapenzi ni Upendo**

Upendo na mapenzi ni vitu ambavyo vinakwenda sambamba na pale ambapo kimojawapo kinakosekana kingine hakiwezi kuwapo. Upendo ni kitu ambacho kinaweza kuleta mapenzi ya kweli baina ya watu wawili wanaopendana.Katika hali ya kawaida, watu wanaopendana hawawezi kuyumbishwa au kufitinishwa na mtu mwingine yeyote asiyependa kuwaona wanaishi vizuri katika maisha yao ya kila siku. Ramadhani (2013) anaeleza kuwa upendo ni ile hali ya mtu kuwa na mapenzi ya dhati kwa mwenzi wake kwa kumvumilia, kumjali, kumheshimu, kumsaidia kwa hali na mali na kumwezesha kufikia matarajio yake katika maisha. Kwa hakika watu wawili wanaopendana ni lazima watendeane mambo haya, tena kwa moyo mkunjufu na ndipo wanapoweza kudumisha mapenzi yao na kuwashinda wafitini (Khamis, 2004). Mzee Yufuf Mzee katika wimbo wake wa *Linawachoma* katika ubeti wa nne na kiitikio cha wimbo huu anasema:

Kuumwa mtaumwa kweli, kwa pendo hili linawachoma
Lawakera kikweli kweli, nyie msotaka kukoma
Mna nyuso za kikatili, na roho zenu za chuma
Gumu sana pendo hili, bure hayo mnosema
Pendo letu la asali, hulia kijiko si uma
Taabani zetu hali, vifua vyetu vyahema
Hakuniona chakula hali, hakimpiti anasema
Tumeshafunga kufuli, tutapendana daima
…
Enyi ee enyi ee enyi ee, wakaanga sumu
Poleni poleni, poleni kwa yalo wasibu,
Pendo letu hili gumu, halipati majaribu

Katika ubeti huu mtunzi anaonesha kuwa upendo baina ya wawili wanaopendana na hususani mke na mume, ni kitu cha muhimu sana chenye kuwezesha kuwashinda wafitini na kudumisha mapenzi yao. Msanii anasema “pendo letu la asali, hulia kijiko si uma,” kwa lengo la kutoa msisitizo wa kuonesha namna ambavyo wawili hao ambao ni Mzee Yusuf na mkewe wanavyopendana kwa dhati kiasi kwamba hakuna mtu yeyote mwenye uwezo wa kutenganisha mapenzi yao. Kimsingi, asali ni aina ya kimiminika ambacho hutengezwa na nyuki na kina sukari iliyokowa na kuwa tamu kuliko vitu vyote vyenye utamu wa sukari katika jamii. Kulifananisha pendo sawasawa na asali ni kuonesha kuwa pendo hilo ni la dhati na hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kuliteteresha (Khamis, 2001).

Imetokea katika jamii kuona mtu na mpenzi wake wakiitana kwa neno la Kiingereza, "Honey," ikiwa na maana ya asali. Hii inamaanisha kuwa wapenzi hao wanaitana kwa jina la asali.

Kwa kuzingatia mawazo ya nadharia ya Saikolojia Changanuzi, inaelezwa kuwa wapenzi wanapoitana majina mazuri huzifanya akili zao, na kwa jumla saikolojia zao, kutulia na kuwafanya wapendane zaidi (Ahearn, 2001). Kuzungumza maneno na kuitana kwa majina mazuri huwafanya wapenzi kuwa na uhakika kuwa kila mmoja anapendwa na mwenzake na hivyo kutosikiliza maneno kutoka kwa mtu yeyote yule mwenye nia ya kuwachonganisha.

Katika msitari wa mwisho wa sehemu ya kiitikio iliyopo hapo juu, mtunzi anasisitiza kuwa pendo ndio kitu cha pekee ambacho kinaweza kudumisha mapenzi baina ya mke na mume. Katika msitari huo anasema, "pendo letu hili gumu, halipati majaribu," akiwa na maana kuwa penye pendo hakuna mtu ambaye anaweza kupenyeza fitina na ikapenya. Mtunzi amaetumia maneno, "pendo letu hili gumu," akiwa na maana kuwa upendo huimarisha mapenzi na kusadia sana katika kudumisha ndoa katika jamii. Katika jamii nyingi za Kitanzania, kumekuwa na matatizo makubwa ya ndoa kutokana na kukosekana upendo baina ya wanandoa na wanajamii kwa jumla. Kukosekana kwa upendo katika familia hufanya ndoa nyingi kuvunjika kutokana na maneno ya fitina yanayoletwa na watu wasiopenda kuona ndoa za watu zinadumu. Suluhisho pekee la kuepusha ndoa nyingi kuvunjika ni kuhakikisha kuwa upendo unadumishwa katika jamii na pia kwa kila mtu na mpenzi wake. Mapenzi hukaa mahali penye upendo na kamwe hayakai mahali penye chuki na fitina (Fisher, 2004).

**2.2 Mapenzi na Fitina**

Katika sehemu iliyotangulia hapo juu, tumebainisha namna upendo unavyoweza
kudumisha mapenzi na kuimarisha ndoa dhidi ya fitina. Katika sehemu hii tunataka kuonesha ni kwa vipi katika mapenzi fitina inajitokeza na kuweza kuhatarisha kudumu na kuimarika kwa mapenzi ya mke na mume. Katika hali ya kawaida, wanadamu walio wengi huwa hawapendi kuona watu wanaopendana, wanadumu katika mapenzi yao na hivyo hufanya kila hila ili kuhakikisha wanatengana au kuchukizana (Fisher, 2006). Hii inalezwa hata katika vitabu vitakatifu vya dini kuwa wapo baadhi ya watu ambao huchukua maneno ya uchonganishi na kuyapeleka kwa watu wanaopendana ili kuvunja mapenzi yaliyopo baina ya watu wawili hao. Mzee Yusuf Mzee anathibitisha suala hili katika wimbo wa *Nitadumu Naye* pale anaposema:

Sijui nipewe nini, kwake nishatosheka
Huyu ndiye wangu ayuni, hana hofu sina shaka
Hata niambiwe nini, kwengine sendi teseka
Kwake ninakosa nini, napewa ninachotaka
Ikiwa cha bakulini, nachota pasi na shaka
Kiwe ndani ya sahani, hunilisha muhibaka
Simuachi asilani, wanochonga nawataka
Wako wanoniambia, ana hivi ana vile
Nitadumu naye ishaallah, kwa mola Baraka tele
Anajulia mashaallah, tena ana sifa tele
Kwa tabia hana ila, na tumbo lake teule
Nampenda kila mahala, kienda huku na kule
Penzi letu la muala, si kama penzi la wale
Kiulaini nakula, furaha yetu milele.

Wako wanaotamani, penzi kutuvurugia
Hawawezi asilani, wala wasiingilie
Labda nife nende kaburini, au afe nimzike yeye
Mapenzi yetu ya shani, raha na mambo yake oye
Nampenda kama nini, sijaona kama yeye
Kwake karaha sioni, raha pendo letu siye
Cheko bashasha usoni, Ishaallah nitadumu naye.

Katika ubeti wa kwanza hapo juu, mtunzi ameanza kueleza kuwa yeye binafsi anaridhika na kila kitu ambacho mpenziwe anampatia na hivyo hana sababu ya kutengana na mpenziwe huyo. Pamoja na kupatiwa kila kitu anachotaka kutoka kwa mpenzi wake lakini wafitini hawakosekani, kwani katika ubeti wa pili anaonesha namna fitina zinavyoanza kuwagombanisha. Katika msitari wa kwanza wa ubeti wa pili mtunzi anasema, "wako wanoniambia, ana hivi ana vile," kauli inayoonesha fitina tayari imekwishaanza. Hili ni jambo la kawaida sana katika jamii ambapo suala la baadhi ya watu kusema maneno ya uzushi dhidi ya watu wanaopendana lipo. Watu wa aina hii hakuna jambo lolote la maana wanalotaka zaidi ya kuona wanaopendana wamehitilafiana na hawaishi pamoja tena (Khamis, 2007). Hali hii inapotokea wao hufurahi sana.

Kimsingi, suala la kuwafitinisha watu wanaopendana ili waharibu mapenzi yao ni suala la kisaikolojia. Tunasema ni suala la kisaikolojia kwa sababu pale tu akili ya mmoja kati ya wapendanao inapokubaliana na maneno kutoka kwa wafitini husababisha ugomvi mkubwa na mpenzi wake na kisha kuvunjika kwa mapenzi yao (Naumann, 2001). Vile vile, suala la mmoja au wote baina ya wapendanao kutokukubaliana na maneno ya wafitini dhidi ya penzi lao ni tukio la kisaikolojia pia. Katika msitari wa pili wa ubeti wa pili, mtunzi anasema, "nitadumu naye inshaallah, kwa mola Baraka tele." Hii inaonesha kuwa saikolojia ya mmoja kati ya watu wawili wanaopendana haikukubaliana na maneno ya wafitinishaji na hivyo kuendelea kudumisha mapenzi yao bila ya kujali maneno ya watu. Si hivyo tu, bali pia, katika ubeti wa tatu mtunzi anaonesha kuwa fitina katika mapenzi ni kitu ambacho kiko bayana. Anasema, "wako wanaotamani, penzi kutuvurugia," akiwalenga wafitinishaji. Suala

hili pia ni tukio la kisaikolojia kwa wafitinishaji husussani pale wanapokamilisha fitina nyoyo na nafsi zao hujisikia vizuri sana (Giddens, 1992).

Hivyo basi, katika kudumisha mapenzi baina ya watu wawili wanaopendana ni lazima wahusika wahakikishe kuwa hawaikubalishi saikolojia yao kwa maneno yanayosemwa na wafitini. Ikiwa kila mwanajamii ataepuka maneno ya wafitini ni wazi kuwa ataishi katika mapenzi yenye upendo na amani. Maisha yenye upendo baina ya watu wawili wanaopendana yatategemea saikolojia yao katika kukabiliana na maneno ya watu wasiowatakia maisha mema. Mtunzi anathibitisha hali hii katika wimbo wa Linawachoma katika ubeti wa pili kuwa:

Sina la kuwaambia, ila pendo letu linawachoma
Siku wanatuhisabia, mwezi na mwaka mzima
Wapo wanotuambia, nyie hamna mwisho mwema
Na sasa wameamua, kuleta nyengine njama
Pendo kutuvurugia, kwa maana linawachoma
Kwetu mtamaliza njia, sisi tunawatazama
Labda mola kiamua, hapo sina la kusema
Na ishaallah atatuvua, husuda zenu na njama

Dondoo hili linaonesha namna mtunzi alivyoikubalisha saikolojia yake ya kwamba haiwezi kuyumbishwa na kukubaliana na maneno ya husuda yanayosemwa dhidi ya mpezi wake. Kutokana na hali hii, si rahisi kwa mtu yeyote yule kuweza kuwatenganisha wawili hao kwa sababu tayari wameshaamini kuwa kila jambo linalosemwa dhidi ya mmoja wao ni la uongo na halina ukweli wowote. Mtunzi anasema, "labda mola kiamua, hapo sina la kusema," akiwa na maana kuwa mwenye uwezo wa kumtenganisha yeye na mpenzi wake ni Mwenyezi Mungu peke yake. Katika maisha ya kila siku ya jamii, ni watu wachache sana ambao wanaweza kuifanya saikolojia yao kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mwenye uwezo wa kila kitu na mwanadamu hana ujanja wala uwezo wa kuvunja mapenzi ya watu wanaopendana. Tunasema hivi kwa sababu wengi katika jamii huifanya saikolojia yao kukubaliana na yale yanayosemwa na watu dhidi yao na hatimaye kuvunja ndoa zao (Traore, 2004). Jambo hili si jema na linapaswa kutafakariwa kwa kina na wanandoa na watu wengine wote wanaopendana ili waweze kudumisha mapenzi yao mpaka pale Mwenyezi Mungu atakapowatenganisha kwa kifo.

**2.3 Mapenzi ni Kujiamini**

Suala la kujiamini na kuaminiana katika mapenzi ni jambo la muhimu katika kuhakisha kuwa watu wawili wanaopendana wanadumu katika mapenzi yao. Kujiamini ni hali ya mtu kuwa na uhakika wa kila anachokifanya kwa mpenzi wake kuwa ni kitu muafaka na bila shaka kitamfurahisha mpenzi wake kwa namna moja au nyingine. Sambamba na hilo, kujiamini pia ni ile hali ya wapenzi kuwa na uhakika kuwa anao uwezo wa kufanya mambo anayotakiwa kumfanyia mwenzi wake kwa kiwango kile kinachotakiwa ili baadaye mambo yao yaweze kuwa mazuri zaidi. Kujiamini katika mapenzi ni suala la msingi sana ambalo kwalo mapenzi ya watu wawili wanaopendana yanaweza kudumishwa zaidi na zaidi. Mzee Yusuf Mzee amelitambua suala hili na katika wimbo wake wa *Najiamini* anasema:

Naomba kheri, mwenye nguvu ni mola ni mola
Nayatanguliza haya, kwa kuwa anajua tangu
Najiamini kwa uwezo, niliopewa na Mungu
Najiamini kwa penzi, nilompa namridhia
Labda awe mpuuzi, ujinga alozoea
Kwa niliye naye, najiamini kwa sana
Tena najijuwa, mimi nampenda sana
Naye ananipenda sana.
Najiamini huyu katulia, najiamini kwa moyo na macho
Sioni tabu na sitomtoa, na chochote nitokuwa nacho
Roho yangu malkia, karidhika na nilichonacho
Nampenda my dear, na waumwe wenye vijicho
Mikononi mwangu katulia, niwe sina niwe nacho
Hata tukilala njaa, honey huweka kificho
Najiamini popote, atakapokwenda huridhia
Kweli wabaya si wote, wahenga wametuambia.

Katika ubeti wa kwanza hapo juu mtunzi anaonesha kuwa kujiamini katika mapenzi ni jambo la msingi linalopaswa kuzingatiwa na kila mwanajamii. Kwanza, mwanamume anatakiwa ajiamini kuwa amepewa uwezo na Mwenyezi Mungu wa kuweza kumtimizia mpenzi wake mahitaji yake yote ya kila siku. Akijiamini katika hili tayari ataifanya saikolojia yake kuona kila jambo ni jepesi hata kama ni zito kiasi gani. Suala la kujiamini kwa mwanadamu linamchango mkubwa katika kuifanya akili ifanye kazi kwa juhudi na maarifa na hatimaye kufanikiwa katika maisha (Ahearn, 2001). Mtunzi anasema, "najiamini kwa uwezo, nilopewa na mungu," ikiwa ni kauli ambayo tayari inamweka mhusika katika saikolojia ya kufanya juhudi na maarifa katika kila jambo analolifanya ili kudumisha na kuendeleza mapenzi yao.

Katika ubeti huo huo wa kwanza katika msitari wa pili mtunzi anasema, "najiamini kwa penzi, nilompa namridhia," akiwa na maana kuwa mapenzi anayompatia mkewe ni muafaka na ndiyo yanayotakiwa na mkewe huyo. Kwa hakika, mtu ambaye anajiamini katika jambo mara nyingi hufanikiwa kulitekeleza jambo hilo kwa uhakika na ufanisi wenye tija ndani yake. Hakuna jambo baya kama kutokujiamini katika mapenzi. Jambo hili lina athari mbaya kisaikolojia hasa pale mtu anapokosa kujiamini kila mara hudhani kuwa anaibiwa au anasalitiwa na mpenzi wake (Sternberg, 1986). Imani kama hii husababisha watu wawili wanaopendana kulumbana kila mara na hatimaye kusababisha mapenzi yao kutodumu kwa muda mrefu. Mtunzi katika ubeti wa pili, msitari wa kwanza hapo

juu, anasema kuwa, "najiamini huyu katulia, najiamini kwa moyo na macho," ikiwa na maana kuwa ni vema katika mapenzi watu wakaaminiana. Kuamini kuwa mpenzi wake mtu ametulia yaani, hana uhusiano wa kimapenzi na mtu au watu wengine tofauti na mpenzi wake, ni jambo lenye kurutubisha upendo baina ya watu wawili wanaopendana (Khamis, 2012).

Kimsingi, mambo yanayoelezwa katika dondoo lililopo hapo juu yanatokea katika
ulimwengu halisia wa maisha ya kila siku ya jamii. Si jambo la ajabu kuona mwanamme au mwanamke akimfuatilia mpenzi wake ili kubaini kama ana uhusiano na mtu mwingine nje ya ndoa au uhusiano wao. Kwa mujibu wa maelezo ya wanasaikolojia, mtu wa aina hii hukosa utulivu wa nafsi na hivyo kutoweza kufanya kazi au mambo yake kwa ufanisi (Davis na Boudreaux, 2010). Hii inatokana na ukweli kwamba, kila jambo ambalo atakuwa analifanya, akili na mawazo yake hayatakuwa katika jambo hilo bali juu ya kusalitiwa na mkewe. Waswahili husema kuwa hakuna jambo linalotesa na kusumbua akili ya mwanadamu kama kutokuelewana kwa watu katika mapenzi yao. Hii inathibitishwa na maelezo ya Sigmund Freud kuwa mapenzi au raha ya kijinsia ndio kitu ambacho kinachukuwa nafasi kubwa katika saikolojia ya mwanadamu. Hivyo, mwanadamu anapotatizika kidogo, hususani kuhusu mapenzi, akili na saikolojia yake kwa jumla huvurugika kabisa. Baadhi ya watu wanaokumbwa na hali kama hii huweza kupata matatizo ya akili na kuwa vichaa. Kwa msingi huo, ni vema wapenzi wakajenga tabia ya kuaminiana baina yao ili mmoja wao asije akafikia hali kama hii.

**2.4 Mapenzi na Dua**

Dua ni maombi maalumu yanayofanywa na mwanadamu kwa Mola wake ili aweze kufanikiwa katika jambo au mambo yake anayokusudia kuyafanya. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuwa anatarajia kuanza kufanya mtihani wake wa kuhitimu masomo au muhula. Ili kuweza kufanikiwa kumaliza mitihani yake na kufaulu vizuri, hulazimika kuomba dua kwa Mwenyezi Mungu kwa lengo la kupatiwa afya njema katika kipindi chote cha mitihani. Kwa kuwa tukio la kuomba dua ni la kisaikolojia, ni dhahiri kuwa muombaji hupata ujasiri na nguvu ya kufanya jambo alilokusudia na kupata mafanikio aliyoyataraji hata kama si kwa ukamilifu wake (Naumann, 2001). Kuomba dua ni tendo linalofanywa na wanadamu wa dini na madhehebu mbalimbali kila mmoja kwa imani yake. Kimsingi, "dua" ni neno lililozoeleka kutumiwa na watu wenye imani ya Kiislamu huku "maombi" likiwa ndilo neno linalotumiwa sana na Wakristo.

Mwimbaji maarufu wa nyimbo za taarab ya mipasho, Mzee Yusuf Mzee anatueleza kuwa hata katika mapenzi kunahitajika kufanywa dua ili kumuomba Mungu ayadumishe mapenzi ya wawili wanaopendana kama yeye na mkewe. Katika wimbo wake wa *Tupendane* anasema:

Siku zote wakuombwa ni Mungu
Yetu sote anopanga ni Mungu
Hao maadui zetu, wanafanya kila hila
Na hili penzi letu, linalindwa na Mola
Hatuwapi nafasi, nyuma wakaturejesha
Hao wapambe nuksi, jeuri tutawaonesha
Kutwaa tunaomba Mungu, wasijeleta majungu
Tunapendana kizungu, kwa matamu na machungu.

Oooh mpenzi wangu, wabaya wetu macho watukodolea
Oooh tuzidi kuomba Mungu, penzi letu lizidi kumea
Honey nataka unibebe, unipeleke kuoga
Sweety nilishe nishibe, hata mlo uso mboga
Kisha nikupe kila kitu, ulichohalalishiwa
Nami nikupe mavitu, mwenyewe unanijua
Kisha tucheze sebene letu, mpaka jogoo anatua
Kwa kila mbaya wetu, kituona atazimia.

Mzee Yusuf Mzee katika ubeti wa kwanza wa wimbo wake hapo juu, anaonesha kuwa ili ndoa au penzi la watu wawili wanaopendana liweze kudumu, ni lazima watu hao wajitahidi sana katika kumuomba Mwenyezi Mungu. Kumuomba Mwenyezi Mungu ndio nyenzo na kinga imara dhidi ya watu wenye kufitinisha ndoa na mapenzi ya wawili wanaopendana. Mtunzi anasema, "siku zote wakuombwa ni Mungu, yetu sote anopanga ni Mungu," akiwa na lengo la kutoa msisitizo juu ya umuhimu wa kumuomba Mungu ili aepushilie mbali fitina kutoka kwa wafisidi. Msisitizo huu unatoa mwelekeo kuwa si jambo la busara kwa watu wanaopendana kwenda kwa waganga ili kupatiwa kinga dhidi ya wafitinishaji (Mzee, 2011). Kuamini kuwa Mwenyezi Mungu ndiye muweza wa kila jambo, ni tukio la kisaikolojia na kuamini pia katika uganga wa kishirikina na nguvu za kiza kuwa ndizo ziwezazo kila kitu ni tukio la kisaikolojia pia.

Hata hivyo, kuamini na kuomba dua, maombi au sala kwa Mungu ni jambo jema zaidi ikilinganishwa na imani za kishirikina na nguvu za giza (Phillip, 2009). Katika kuthibitisha hili, mtunzi anasema, "hao maadui zetu, wanafanya kila hila, na hili penzi letu linalindwa na Mola."Hapa mtunzi anaonesha kuwa kulikabidhi penzi lilindwe na Mwenyezi Mungu ni jambo muafaka katika kuhakikisha penzi hilo linadumu milele na milele. Kulikabidhi penzi kwa Mungu si kwa maneno tu bali kufanya maombi na dua kila siku. Mtunzi anasema, "oooh tuzidi kuomba Mungu, penzi letu lizidi kumea," akiwa na maana kuwa, kumuomba Mungu ili adumishe penzi la wanandoa ni kitu endelevu na kadiri muombaji anavyozidi kuomba, ndio anavyopata ulinzi imara kutoka kwa Mungu.

Kimsingi, katika maisha halisia ya jamii tumeona baadhi ya

wanajamii wakifanya jitihada kubwa katika kufanya dua na sala zenye lengo la kumuomba Mwenyezi Mungu ili adumishe mapenzi waliyonayo na wapenzi wao. Tunaona dua na maombi yakifanyika kwa mikesha ya siku kadhaa na lengo likiwa ni hilo la kumuomba Mungu kuwa ndiye mlinzi wao. Maelezo ya nadharia ya Saikolojia Changanuzi yanasema kuwa, mwanadamu ni kiumbe anayependa kuishi katika maisha ya amani, utulivu, mapenzi na upendo. Hivyo, anapomuomba Mungu kuwa ndiye mlinzi wa penzi dhidi ya maadui, ni njia ya kujihakikishia amani, usalama, upendo na mapenzi katika familia na jamii kwa jumla. Hivyo, ni jambo jema kwa wanajamii kuhakikisha kuwa wanajikita katika kufanya ibada kila siku ili kuomba ulinzi wa mapenzi yao dhidi ya mafisadi kutoka kwa Mungu.

**2.5 Mapenzi ni Kutendeana Wema**

Kutendeana wema katika mapenzi ni kitu cha msingi chenye kustawisha na kunawirisha penzi la watu wanaopendana akiwemo mke na mume. Kutendeana wema ni ile hali ya wapenzi kufanyiana ukarimu na kuwa na mtazamo chanya juu ya mwenzi kuhusu mambo mbalimbali katika maisha yao ya kila siku. Kwa mfano, mwanamume analazimika kumpatia mkewe mahitaji yake yote ya kila siku kama vile chakula, mavazi, malazi na fedha za matumizi yake binafsi, ikiwemo kununua manukato na mahitaji mengine ya mwanamke. Kufanya mambo haya ni kumtendea wema mkewe. Kwa upande wa mwanamke naye anapaswa kumtendea wema mumewe kwa kuhakikisha kuwa mumewe anapata mahitaji yake yote yanayotakiwa kutekelezwa na mwanamke. Miongoni mwa mahitaji hayo ni pamoja na kupika chakula, kumkanda mumewe, kumlisha chakula, kufua nguo, kusafisha nyumba na kuwalea watoto katika misingi mizuri kimaisha (Ramadhani, 2013).

Mtunzi na mwimbaji maarufu wa nyimbo za taarab ya mipasho Mzee Yusuf Mzee ameliona suala la kutendeana wema katika mapenzi ni muhimu sana katika kudumisha mapenzi ya mke na mume. Katika wimbo wake wa *VIP Soda ya Kopo* anasema:

Wanaume tumepewa, daraja kubwa kwa Mungu
Mashababi tunakuwa, na kila aina ya Mizungu
Ila unapozidiwa, huna ujanja mwanangu
Mimi ninavyoenziwa, first class wenzangu
Vile nnavyo hudumiwa, nimepanda daraja yangu
Penye sifa husifiwa, VIP nafasi yangu
Nikitaka kula, ninalishwaa
Nikitaka kunywa, ninanyweshwaa
Nikitaka kunawa, nanawishwaa
Na pia kuoga, naogeshwaa
Jamani nahudumiwa, raha hadi utosini
Nnachotaka nnapewa, niseme nataka nini
Raha singoji kupewa, najipa mwenyewe jamani
Naona ntachelewa, kidume kula maini
Chakula nnapikiwa, nnawekewa mezani
Nikila napepewa, kishuke vyema tumboni
Sigombwi mimi nadekezwaa
Na nikiumia napulizwaa
Kufanya utundu, nakatazwaa
Siwahi kusema, naulizwaa.

Katika dondoo hili mtunzi anaonesha kuwa wema ambao unapaswa kufanywa na mwanamke kwa mumewe ni ule usiokuwa na kipimo kwa lengo la kudumisha ndoa yao. Hili linathibitika pale anaposema, “nikitaka kula ninalishwa, nikitaka kunywa ninanyweshwa, nikitaka kunawa nanawishwaa na pia kuoga naogeshwa.” Bila shaka mwanamume kufanyiwa mambo yote haya na mwanamke ni wema usiokuwa na kipimo wala mipaka. Mwanaume yoyote anayefanyiwa mambo kama haya na mkewe, inakuwa ni vigumu sana kumwacha mkewe akateseka bila ya kumpatia mahitaji yake ya kila siku (Rahim, 2002). Kwa mujibu wa nadharia ya Saikolijia Changanuzi, mwanamume anayeenziwa na mkewe kwa kufanyiwa mambo haya, hupata utulivu wa moyo na nafsi na kujiona kuwa yeye ni mfalme katika dunia. Kwa maana nyingine ni sawasawa na kusema kuwa mwanamume huyo hupumbaa na kila kitu ambacho ataambiwa na mkewe huyo atakubali bila ya pingamizi lolote (Sternberg, 1986). Baadhi ya watu humwita mwanamume wa aina hiyo kuwa amepewa limbwata na mkewe. Hata hivyo, hakuna ukweli wowote juu ya limbwata hilo bali ni yale mambo ya wema na ukarimu afanyiwayo mwanamume na mkewe ndio yaliyomlainisha na kumsikiliza mkewe kwa kila jambo.

Katika ubeti wa pili hapo juu, mtunzi anatuonesha kuwa kutendeana wema baina ya mke na mume ni pamoja na mwanamke kumpikia mumewe chakula na kumwandalia. Anasema, “naona ntachelewa kidume kula maini, chakula napikiwa nnawekewa mezani.” Kauli hii inaonesha kuwa miongoni mwa mambo ya mke kumtendea wema mmewe ni kumwandalia chakula kizuri zaidi kuliko watu wengine wote katika familia. Kula “maini” kunakosemwa hapo juu kunamaanisha chakula chochote kizuri na chenye ubora wa hali ya juu ndicho alichoandaliwa mwanamume. Saikolojia ya mwanamke imejengeka kuamini kuwa mume ni mtu anayestahili kula kitu kizuri zaidi kuliko hata yeye mwanamke mwenyewe anayepika chakula (Fisher, 2006). Kwa mfano, kama chakula cha siku husika ni wali na nyama ya kuku basi mwanamume atapatiwa sehemu ya kuku yenye nyama zaidi kuliko sehemu nyinginezo. Anaweza kupatiwa sehemu ya paja, kidari na kipapatio.

Saikolojia hii haiko kwa wanawake peke yao bali hata kwa wanaume pia ambapo nao huamini kuwa wao ndio wanaostahili kupatiwa kila kilicho bora zaidi. Kutekelezwa kwa mambo haya ni moja kati ya

kutendeana wema baina ya mke na mme na kwa njia moja au nyingine husaidia kudumisha mapenzi.

Vile vile, mtunzi katika dondoo lililopo hapo juu anaendelea kuonesha kuwa kutendeana wema baina ya mme na mke ni pamoja na kuelekezana juu ya masuala mbalimbali kwa kutumia lugha nzuri isiyokuwa ya karaha. Anasema, "sigombwi mimi nadekezwa," ikiwa na maana kuwa mtu anapokosea huelekezwa kwa namna ambayo si ya kukaripiwa wala kuudhiwia. Katika hali ya kawaida, hakuna binadamu ambaye ni mkamilifu kwa kila kitu na asiwe ni mwenye kukosea. Hata hivyo, anapokosea ni lazima aelekezwe na kuonywa kwa wema ili aweze kuelewa na siku nyingine asirudie tena. Neno "kudekezwa" lilivyotumiwa hapa linamaanisha lugha ya upole, taratibu, busara na hekima. Neno hili halijatumiwa kurejelea hali ya mtu kufanya makosa na kuachwa bila ya kuonywa na hivyo kila siku kuendelea na tabia yake hiyo ambayo si mujarabu. Katika taaluma ya Saikolojia, kunaelezwa kuwa mwanadamu ni kiumbe anayejifunza na kuelewa zaidi katika muktadha ambao si wa kukaripiwa au kusemwa kwa maneno ya kejeli na kashfa (Davis na Boudreaux, 2010). Hivyo, kuelekezana kwa lugha ya upole na ukarimu baina ya mke na mme juu ya mambo mbalimbali katika familia yao ni muhimu sana katika kuimarisha mapenzi yao. Haya yanaweza kufanyika pale tu ambapo kutendeana wema baina ya mke na mume kumepewa nafasi katika maisha ya kila siku.

**2.6 Mapenzi na Tabia Nzuri**

Tabia ni mwenendo wa mwanadamu katika utendaji wake wa shughuli mbalimbali katika jamii tangu anaamka asubuhi mpaka anapolala usiku. Mwenendo huo upo katika aina mbili ambapo ni mwenendo mzuri na mwenendo mbaya. Mwenendo mzuri ndio huitwa tabia nzuri na mwenendo mbaya huitwa kuwa ni tabia mbaya. Mapenzi ni kitu ambacho kinahitaji kuenziwa na kudumishwa kwa waliopo katika mapenzi kwa kuwa na tabia nzuri zenye kukubalika kwa wao wenyewe na kwa jamii pia. Kwa mfano, mwanamke mwenye tabia nzuri ni yule ambaye anaomba ruhusa kwa mumewe kila mara anapotaka kwenda mahali popote nje na nyumbani kwao. Inapotokea mwanamke anakuwa na tabia ya kuamua kuondoka tu nyumbani bila hata ya kuomba rusuha, huhesabiwa kuwa ni mwanamke mwenye tabia mbaya. Mzee Yusuf Mzee ameliona suala hili na amelisawiri vizuri katika wimbo wake wa *Valentine Day* pale anaposema:

She is Cute for me, kila idara ananivutia
Laini nyama ya ulimi, mpole zake tabia
Kwa utulivu sisemi, hatoki bila kunambia
Hali bila kula nami, hakimshuki hunambia, you can't believe
Ananisugua nasugulikaa
Ananiliwaza naliwazikaa
Ananitomasa natomasikaa
Ananituliza natulizikaa.

Dondoo hili linaonesha kuwa miongoni mwa mambo yanayoonesha kuwa mwanamke ana tabia nzuri ni pamoja na kuomba ruhusa au kuaga pale anapotaka kutoka nyumbani. Hii ni njia nzuri ya kudumisha mapenzi na upendo katika familia. Mtunzi anasema, "kwa utulivu sisemi, hatoki bila kunambia," akiwa na maana kuwa mwanamke mwenye tabia nzuri ni yule ambaye ni mtulivu na hutulia nyumbani kwake si kiguu na njia. Mwanamke mwenye tabia hii humfanya mumewe amwamini na kila mara atakapokuwa anaomba ruhusa ya kwenda mahali atakubaliwa. Saikolojia ya mwanamme ina amini kuwa mkewe anapoomba ruhusa ya kwenda mahali anajali kuwa mume ndiye kiongozi na mwenye mamlaka ya mwisho katika familia (Naumann, 2001). Hivyo, mwanamume anapoombwa ruhusa na mkewe ya kwenda mahali huona fahari kubwa ya kuheshimiwa na mkewe. Inapotokea mwanamke anaamua kuondoka tu nyumbani bila ya kuomba ruhusa kwa mumewe, mume hudhani kuwa amedharauliwa na kwamba yeye si mwenye maamuzi katika familia bali ni mke ndiye mwenye maamuzi (Khamis, 2012). Baadhi ya wanajamii wanapoona hali kama hii hudai kuwa mwanamme ambaye mkewe anaweza kutoka bila ruhusa yake (mume) ametawaliwa na mke. Jambo hili si zuri na husababisha mapenzi ya wanandoa kuyumba na hata wakati mwingine kuvunjika kwa ndoa.

Mahali pengine katika dondoo hapo juu, mtunzi anaeleza kuwa mwanamke anatakiwa kupambika kwa tabia ya upole. Suala la mwanamke kuwa mpole ni la kimaumbile ambapo wanawake wengi hawana tabia ya ubabe na ukorofi kama ilivyo kwa wanaume. Hata hivyo, hii haimaanishi kuwa hakuna wanawake wakorofi na wababe katika jamii. Mwanamke anapokuwa mpole, hata kama mumewe ni mkorofi husaidia ukali na ukorofi wa mume kupoa na mara nyingine kumfanya mume naye kuwa mpole. Mtunzi anasema, "laini nyama ya ulimi, mpole zake tabia," akimtaja mwanamke anapaswa kuwa na maneno mazuri sambamba na kuwa mpole. Upole ni tabia inayoambatana na kauli nzuri kutoka kwa mtu mmoja kumfanyia mwenzake. Katika kuonesha kuwa mwanamke mpole hukuza mapenzi katika nyumba yake, mtunzi anasema, "kama sumu korogeni, lakini hatuachani," akiwa na maana kuwa ndoa yenye mwanamke mpole hudumu na hata wafitini wafanye mambo gani, kamwe hawawezi kuvunja mapenzi ya wawili hao. Katika jamii ya leo kuna mifano hai inayoonesha kuwa katika mapenzi ambapo mwanamke anapokuwa mpole mapenzi yao hudumu kuliko ndoa zenye wanawake wakorofi na wababe.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa taswira ya mapenzi inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za taarab za waswahili. Taswira

hizo ni mapenzi ni upendo, mapenzi na fitina, mapenzi ni kujiamini, mapenzi na dua, mapenzi na kutendeana wema na mapenzi na tabia nzuri. Mtunzi anabainisha kuwa ili mapenzi ya watu wawili wanaopendana yaweze kudumu na kuimarika, ni lazima watu hao wawe na upendo baina yao. Haya yanapatikana katika wimbo wa Linawachoma ambapo inaelezwa kuwa watu wengi katika maisha hawapendi kuona watu wanaopendana wanadumu katika mapenzi yao. Hata hivyo, anasisitiza kuwa kupendana na kuzidisha mapenzi yao ndio njia madhubuti ya kuimarisha mapenzi. Kwa hakika, hivyo ndivyo saikolojia ya mwanadamu ilivyo, kwani hupenda kuona watu wakiishi maisha ya chuki badala ya upendo.

Sambamba na hilo, pia taswira ya mwanamke inajitokeza katika masuala ya fitina ambapo baadhi ya watu hufanya fitina ili wapendanao waachane. Kupitia wimbo wa *Nitadumu* Naye mtunzi anasema kuwa njia pekee ya kutunza mapenzi ya mke na mume ni kutosikiliza maneno ya wafitini. Ni vema wapendanao wakafahamu kuwa si kila mtu anapenda kuona wanaishi vizuri kwa amani na utulivu.Katika kuhakikisha kuwa wafitini hawapati nafasi ya kuwatenganisha wapendanao, ni wajibu wa wapendanao kuhakikisha kuwa wanaomba dua kwa Mwenyezi Mungu ili awalinde dhidi ya wafitini. Haya yanapatikana katika wimbo wa *Tupendane* ambapo wapendanao wanatakiwa kuyaombea mapenzi yao ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Pia, taswira ya mapenzi na tabia nzuri inajitokeza kwa kiasi kikubwa katika nyimbo za Mzee Yusuf Mzee. Mtunzi anabainisha kuwa tabia nzuri kwa mwanamke ni upole na kutoondoka nyumbani bila kupata idhini au ruhusa kutoka kwa mumewe. Tabia hii ni nzuri na ina mchango mkubwa sana katika kuimarisha mapenzi ya wawili wanaopendana kwa sababu husaidia katika kujenga uaminifu baina ya wapenzi. Haya yanapatikana katika wimbo wa Valentine Day ambapo pia mtunzi anatoa msisitizo kuwa ni vema mwanamke akawa si mtu wa kusema sema maneno mengi bali akawa mpole na mchache wa kusema. Hii ni tabia nzuri ambayo itasaidia kuhakikisha kuwa wawili wanaopendana wanadumu katika mapenzi yao.

Pia katika utafiti huu tumeweza kubainisha mbinu za kisanaa zilizotumika katika kuwasilisha taswira ya mapenzi kuwa ni misemo, takriri, mafumbo, balagha na sitiari. Mbinu hizi za kisanaa zimetumiwa kwa ufundi wa hali ya juu na msanii na kuweza kujenga taswira ya mapenzi baina ya mke na mume. Kwa mfano, kupitia mbinu ya sitiari, mtunzi ameweza kuonesha namna wapendanao wanavyoweza kupeana majina mazuri kupitia vyakula kama inavyojitokeza katika wimbo wa *Tupendane*. Katika wimbo huu, mtunzi ametumia sitiari za “honey” na “sweet,” kama majina anayomuita mpenzi wake. Haya ni majina ya vitu ambavyo vina sukari nyingi inayofanya viwe vitamu sana kwa ulimi wa mnyonyaji au mlambaji. Hata hivyo, hapa majina haya anapewa mwanamke kuonesha kwamba ni mtu mwenye mapenzi ya kumridhisha mumewe.

**MAREJELEO**


**Ahearn**, L. M. (2001), *Invitations to Love: Literacy, Love Letters and Social Change in Nepal*, Ann Arbor: University of Michigan Press.

**Allen**, T. H. (1978), *New Methods in Social Science Research*, New York: Praeger Publication.

**Askew**, K. A. (2000), “Following in Tracks of Beni. The Diffusion of Tanga Taarab Tradition”. Katika F. Gunderson & G Barz (Eds) *Mashindano:Competitive Music Performance in East Africa*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

**Babbie**, E. (2007), *The Practice of Social Research*, Belmont: CA, Wadsworth.

**Boeree**, G. C. (2006), *Personality Theories*, e-text Book.

**Clover**, V. T. and Balsey H. L. (1974), *Business Research Methods*, Columbus: Grid Inc.

**Davis**, P. and Boudreaux, C. (2010), “The Social Pschology of Love and Attraction,” McNair Scholars Journal, Vol. 14, Issue 1 Grand Valley State University.

**Cohen**, A.na Wenzake (2000), *Research Methods in Education*.London: Routledge Falmer.

**Emory**, C. W. (1974), *Business Research Methods*, Illnois: Homewood.

**Farhan**, I. (1992), “History of Taarab Music in Zanzibar,” Paper Presented in InternationalConference on the History & Culture of Zanzibar, SUZA Library.

**Ghosh**, B. N. (1982), *Scientific Methods and Social Research*, New Delhi: Sterling Publishers Pvt. Ltd.

**Giddens**, E. (1992), The Transmissions of Intimancy: Sexuality, Love & Eroticism in Modern Societies, Stanford CA: Stanford University Press.

**Herry**, N. (2002), *Action Research: A Pathway to Action*, *knowledge and Learning*, Melborne: RMIT Publishing.

**Khamis**, S. A. M. (2001), “Redefining Taarab in Relation to Local anda Global Infuences,” In *Swahili Forum*, VIII- pg 145-156.

**Khamis**, S. A. M. (2004), “Images of Love In the Swahili Taarab Lyric: Local Aspects and Global Influence,” *Swahili Forum*, Vol. 111 pg 123-145.

**Khamis**, S. (2005), Clash of Interest and Conceptualiasation of Taarab in East Africa, *Swahili Forum* 12/ 133-159.

**Kothari**, C. R. (2008), *Research Methology, Methods and Techniques*. Second Edition, Delhi: New Age International (P) Ltd.

**Mgana**, I. (1991), *Jukwaa la Taarab Zanzibar*. Mradi wa Mediafrica: Helisinki.

**Mlacha**, S. A.K. (1996), “Women Images in Kiswahili Poetry & Taarab Songs*”,* inD. Mbilinyi & C Omary (Eds): *Gender Relation & Woman Media*.Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

**Mulokozi**, M. M. (1996), *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo

Kikuu Huria cha Tanzania.

**Mzee**, A. F. (2011), Athari za Nyimbo za Mipasho katika Jamii ya Wazanzibar. Tasnifuya M.A, Chuo Kikuu cha Dodoma.

**Naumann**, E. (2001), *Love at First Sight*, Naperville, IL: Sourcebooks, Inc.

**Phillip**, L. (2009), "A Critical Language Study of Mipasho Taarab and Bongo Fleva," Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**Rahim**, U. (2002), *Philosophical Ground of Western Civilization*, New York: Sage.

**Rajasekar**, S. na Wenzake, (2013), *Research Methodology*, Tamilnadu: India.

Traore, F. A. (2004), "Continuity and Change in Zanzibar Taarab Performance and Poetry," in*Swahili Forum* 11/75-84.

**Wamitila**, W. (2003), *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia.* Nairobi: Focus Publications Ltd.

**Wamitila**, W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi.* Nairibi: Phoenix Publishers Ltd.

**Yego**, K. (2013), "Nafasi ya Mwanamke: Jinsi Inavyotetewa katika Nyimbo za Taarab za Zanzibar," Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Nairobi.